

Aina za Madd zinazohusiana na مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) ni:

أَلِفَاتُ السَّبْعِ Alifaatus-Sab-'iy - Alif Saba

Hukmu ya مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) inayopatikana katika maneno saba pekee ya Qur-aan, hutekelezwa pale anaposimamia tu msomaji. Ama akiendelea kisomo, hukmu ya مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) inabatilishwa.

Na hizi zinajulikana kwa jina la أَلِفَاتُ السَّبْعِ (Alifaatus-Sab-'iy - Alif Saba) na alama yake ni kiduara cha umbo la yai juu yake.

Imetajwa katika Qur-aan	Suwhah Aayah	Neno
Mara kadhaa		أَنَا
Pekee	Al-Kahf: 38	لَنَكْنَا
Pekee	Al-Ahzaab: 10	الظُّنُونَا
Pekee	Al-Hazaab: 66	الرَّسُولَا
Pekee	Al-Ahzaab: 67	السَّيْلَا
Pekee	Al-Insaan: 4	سَلْسِلَا
Pekee	Al-Insaan: 15 na 16	قَوَارِيرَا

Mfano: Katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

إِذْ جَاءَكُمْ مِنْ فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنْكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ
بِاللَّهِ الظُّنُونَا ﴿١٥﴾ هُنَالِكَ ابْتُلِيَ الْمُؤْمِنُونَ ...

Aksimama msomaji mwisho wa Aayah katika neno لا الظُّنُونَا atasoma:

... wa idh-zaaghatil-abswaaru wabalaghatil-quluwbul-hanaajira
watadhwunnuwana biLLaahidhw-dhwunuwanaa. Hunaalikab-tuliyal-
muuminuwana....

Bonyeza usikilize

Lakini akiunganisha na neno linalofuatia katika Aayah ya pili yake atasoma:

...wa idh-zaaghatil-abswaaru wabalaghatil-quluwbul-hanaajira
watadhwunnuwana biLLaahidhw-dhwunuwana-hunaalikab-tuliyal-
muuminuwana....

مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) nyinginezo ni:

1. مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى - Maddusw-Swillatis-Sughraa
2. مَدُّ الْعَوَظِ - Maddul-'Iwadhw
3. مَدُّ الْبَدَلِ - Maddul-Badl
4. مَدُّ التَّمْكِينِ - Maddut-Tamkiyn
5. أَلْفَاتُ حَيِّ طَهْرٍ - Alifaatu Hayyun Twahr